# CHRISTON SECONDARY SCHOOL

**P. O. BOX 28055- KISARAWE PWANI**
**CONTACT: 0758498414, 0625931119,**
**Website: www.christonschool.ac.tz, Email: info@christonschool.ac.tz**
**MOTTO: THE FUTURE INSCIENCE**

**REG. NO. S 4824** **EXAM NO. S. 5290**

---

**Fomu Na. ………….**

**FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WAVULANA CHRISTON 2024/2025**

**PICHA**

1. **MAELEKEZO KUHUSU SHULE KWA KIFUPI**
   i. Shule hii ni ya wavulana tu.
   ii. Shule ipo katika Kijiji cha Msimbu (Msangazalala), Kata ya Msimbu, Wilaya ya Kisarawe, Mkoa wa Pwani.
   iii. Shule ni ya bweni tu. (Boarding School).

2. **TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI.**
   a) Jina kamili (majina matatu) …………………………………………………………………
   b) Tarehe ya kuzaliwa …………………………………………………………………………….
   c) Uraia ……………………………………………………………………………………………
   d) Dini ……………………………………………………………………………………………..
   e) Mahali anapoishi ……………………………………………………………………………..
   f) Unajiunga kidato cha …………………………………………………………………………
   g) Jina la shule aliyomaliza darara la saba …………………………………………………………
   h) Namba ya usajili ya mtihani wa darasa la saba (ijazwe ka usahihi)

3. **AFYA (Ijazwe na Mzazi au Mlezi)**
   ❖ Je ana matatizo ya aina yoyote ya kiafya yanayohitaji uangalizi maalumu? (Ndiyo / Hapana)
   Kama ndiyo ni yapi ……………………………………………………………………………

4. **TAARIFA MZAZI / MLEZI.**

i. Jina kamili ……………………………………………………………………………….

ii. Uhusiano na mwanafunzi ……………………………………………………………….

iii. Anapoishi ………………………………………………………………………………..

iv. Anafanya kazi wapi ………………………………………………………………………..

v. Kazi yake ………………………………………………………………………………..

vi. Mawasiliano ……………………………………..…, ……………………………….………..

5. **MASOMO YANAYOFUNDISHWA SHULENI**

BASIC MATHEMATICS, PHYSICS, CHEMISTRY, BIOLOGY, HISTORY, CIVICS, GEOGRAPHY, ENGLISH LANGUAGE, KISWAHILI, MUZIKI NA UJASIRIAMALI.

6. **MITIHANI**

Mwisho wa kurudisha fomu ni tarehe 31/12/2024
Mitihani ya kujiunga itafanyika kila siku ya Jumatatu – Jumamosi kuanzia tarehe 09/09/2024 mpaka tarehe 31/12/2024 kuanzia saa tatu asubuhi shuleni Christon.

7. **AHADI YA MZAZI / MLEZI**

a) Naahidi kuwa mtoto wangu akichaguliwa itambidi afuate sheria, taratibu na maagizo ya shule yatakayotolewa mara kwa mara ili kuboresha taaluma.

b) Iwapo kijana wangu atafaulu mtihani na kuchaguliwa kujiunga na shule, naahidi kulipa kiasi cha shilingi laki tano (500,000/=) kama "Commitment fee" ili kutunza nafasi ya mtoto.

Pesa hiyo inalipiwa kwenye **A/C NO. NMB - 21410017860**

**Jina CHRISTON MEMORIAL EDUCATIONAL INSTITUTIONS LMT.**

**(Andika majina matatu ya mtoto)**

**NB: Malipo yakishafanyika hayarudishwi.**

Sahihi ya Mzazi / Mlezi …………………………………. Tarehe ……………………………

**AUGUST F. MINJA**

**MKUU WA SHULE**

# <u>SHERIA ZA SHULE</u>

**KIAMBATANISHO: SHERIA NA KANUNI ZA SHULE ZISOMWE VIZURI NA KUELEWEKA**

- Kumcha Bwana ni chanzo cha maaarifa Mithali 1:7
- Hekima hupatikana midomoni mwa mwenye ufahamu bali fimbo hufaa kwa mgongo wake asiye na ufahamu,Mithali 10:13
- Mwana mwenye hekima humfurahisha babaye bali mwana mpumbavu ni mzigo wa mamaye Mithali 10:1
- Palipo na kiburi hapakosi aibu bali hekima hukaa na unyenyekevu ,Mithali 11:2 natunapenda kutaarifu kuwa shule haihitaji aibu.

**A: HESHIMA NA UTII**

1. Kila mwanafunzi anatakiwa kusimama na kusalimia mtu yeyote aliyemzidi umri anapopita,anapo ingia darasani au ukumbini.
2. Nimarufuku kutumia lugha ya matusi kwa mtu yeyote.
3. Nilazima kuwaheshimu wafanyakazi wote wa shule kama walezi.
4. Wanafunzi wote washirikiane na kusaidiana katika masomo.
5. Kila mwanafunzi aheshimu na kuthamini kazi za aina zote.
6. Nimarufuku kuvaa mavazi yasiyo na heshima
7. Nimarufuku kufuga ndevu,kucha,vipodozi na mapambo kama herein,mkufu nk.
8. Ni marufuku **kugombana.**
9. Unatakiwa kuitika maramoja na kukimbilia aliko mtu anayekuita.
10. Unatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa na picha za viongozi wa serikali,nembo ya Taifa, Wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.
11. Unatakiwa kuheshimu ukumbi wa mikutano, ofisi za mikutano, mali binafsi,na mali ya umma.
12. Unatakiwa kunyoosha mkono juu na kusimama unapoulizwa au kujibu swali na kukaa kimya unapokuwa darasani usitoke bila ruhusa
13. Nimarufuku kubaguana kisiasa, kidini,kikabila au kitamaduni
14. Nimarufuku kuwa na simu au Radio bila ruhusa
15. Lugha ya mawasiliano ni **<u>Kiingereza</u>** uwapo shuleni hivyo, muda wote unatakiwa kuongea kiingereza. Lugha ya Kiswahili itatumika pindi mwalimu wa somo hilo anapofundisha darasani.
16. Nimarufuku kuingiza chakula bwenini,kuleta chakula cha aina yeyote bila kibali maalumu.

**B: MAHUDHURIO**

1. Unatakiwa kuhudhuria shuleni muda wote wa masomo, endapo utapewa ruhusa ni lazima uwe na kibali kilichosainiwa na patron na mwalimu mmoja au zaidi, akiwepo mwalimu wa zamu. Ikiwa ni zaidi ya siku moja lazima kisainiwe na mkuu wa shule na kama ni ugonjwa basi cheti cha daktari kithibitishe
2. Ni lazima kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa.
3. Unatakiwa kuhudhuria kazi zote za mikono.
4. Unatakiwa kuhudhuria mikutano yote ya shule kama Baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandishwa bendera ya Taifa, mikutano ya bweni na kama itakavyo elekezwa.

**C: MAANDALIYO YA JIONI.**

1. Kila mwanafunzi lazima ahudhurie maandalio jioni (prepo) kwa mda uliopangwa
2. Kila mwanafunzi lazima afanye kazi za darasani na za ziada anazopewa.

**D: KUWAHI**

1. Kila mwanafunzi lazima athamini muda kwa kuutumia ipasavyo kama ilivyopangwa katika ratiba.muda wa darasani, kula, michezo na kulala.
2. Kila mwanafunzi lazima awahi katika shughuli zote kama ilivyopangwa katika ratiba.
3. **Kila mwanafunzi awahi kufungua shule kwa tarehe na muda uliopangwa**.

**E: MIPAKA YA SHULE.**

1. Unatakiwa kutotoka nje ya mipaka ya shule bila kibali maalumu.
2. Kila mwanafunzi lazima afuate tarehe,siku,au saa ya kutoka na kuingia katika mipaka ya shule.
3. Kila mwanafunzi (bweni au hosteli ) lazima awe kitandani wakati wa kuzima taa.

**F: NIMARUFUKU KUTEMBELEA SEHEMU ZIFUATAZO BILA KIBALI MAALUMU.**

A. Nyumba za waalimu na wafanyakazi.
B. Jikoni.
C. Maabara.
D. Ofisi za shule
E. Chumba cha mwalimu.
F. Vilabu vya pombe.
G. Majumba ya starehe au ya kushukia wageni.

**G: USAFI**

1. Kila mwanafunzi ni lazima ahakikishe usafi wa binafsi ( mavazi na mwili na mahali pa kulala, kulia chakula, vyombo vya chakula na mazingira kwa ujumla.

**H: MAKOSA YANAYOWEZA KUKUSABABISHIA KUFUKUZWA SHULE.**

1. Wizi
2. Uasherati na ubakaji
3. Uvutaji bangi
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
5. Kupiga au kupigana
6. Kugoma au kuchochea mgomo/ kuongoza/kuvuruga amani na usalama wa watu
7. Kuharibu makusudi mali ya uma.
8. Kudharau bendera ya taifa
9. Kuoa au kuolewa
10. Kupata mimba au kusababisha nje na ndani ya shule.
11. Kutoa mimba
12. Kukataa adhabu kwa makusudi
13. Makosa ya jinai.

**I: SARE ZA SHULE**

1. Kila mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare za shule kama ilivyoelekezwa sare za michezo, sare za bweni, sare za darasani nk. Muda wote akiwa :.
    a. Darasani
    b. Anapotoka nje ya shule kwa shughuli za shule
    c. Muhadhara wa shule au baraza
    d. **Anapokwenda** hospitali
    e. Maandamano
    f. Anaposafiri kuja shuleni au kwenda kwao
2. Kila mwanafunzi lazima awe na sare za kazi za mikono na michezo na vitumike wakati huo tuu.
3. Kofia na viatu vya gorofa, mabuti na vitambaa vya kichwa haviruhusiwi
4. Sare za shule lazima ziwe safi wakati wote.

***KARATASI HII ITASAINIWA NA KURUDISHWA SHULENI.***

**<u>NB:</u> Makosa mengine hayatatolewa onyo kali, bali kufukuzwa kwa mwanafunzi moja kwa moja.**

Mimi mzazi/mlezi wa……………………………………………nakubaliana na masharti tajwa hapo juu.

Mimi mwanafunzi…………………………………………………. Nakubaliana na kanuni na taratibu tajwa hapo juu.

Sahihi ya mwanafunzi…………………...….Sahihi ya mzazi………………………………..